المجلس الأعلى للشئون الإسلامية بتنزانيا

BARAZA KUU LA WAISLAM TANZANIA ( BAKWATA )

THE NATIONAL MUSLIM COUNCIL OF TANZANIA

# KANUNI ZA JUMUIYA YA VIJANA WA KIISLAMU BAKWATA (JUVIKIBA)

**S.L.P 21422 DAR ES SALAAM**

**TOLEO LA KWANZA MWAKA 2024**

**YALIYOMO**


UTANGULIZI ........ 1

SEHEMU YA KWANZA: TAARIFA YA AWALI YA KANUNI ........ 3

1: JINA LA KANUNI ........ 3

2: TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA ........ 3

3: MATUMIZI YA KANUNI ........ 3

4: TAFSIRI YA MANENO ........ 3

SEHEMU YA PILI: JINA, MAKAO MAKUU NA LUGHA ........ 5

5: JINA LA JUMUIYA ........ 5

6: MAKAO MAKUU YA JUMUIYA ........ 5

7: MAWASILIANO ........ 5

8: LUGHA RASMI ........ 5

9: NEMBO YA JUMUIYA ........ 5

SEHEMU YA TATU: AKIDA, HADHI NA MALENGO YA JUVIKIBA ........ 6

10: AKIDA ........ 6

11: HADHI ........ 6

12: MALENGO YA JUVIKIBA ........ 6

SEHEMU YA NNE: UANAJUMUIYA, HAKI NA WAJIBU ........ 8

13: UANAJUMUIYA ........ 8

14: NAMNA YA KUJIUNGA ........ 8

15: SIFA ZA MWANAJUMUIYA ........ 8

16: HAKI ZA MWANAJUMUIYA ........ 9

17: WAJIBU WA MWANAJUMUIYA ........ 9

18: KUONDOLEWA UANACHAMA ........ 9

19: KURUDISHWA UANACHAMA ........ 10

SEHEMU YA TANO: MUUNDO WA UONGOZI NA VIONGOZI WA JUVIKIBA ........ 11

20: UPATIKANAJI WA VIONGOZI ........ 11

21: SIFA ZA KIONGOZI ..... 11
22: KAMATI KUU ..... 11
23: MAJUKUMU YA KAMATI KUU ..... 12
24: MAJUKUMU YA VIONGOZI ..... 12
25: MIIKO YA UONGOZI ..... 14
26: MUDA WA KUKAA MADARAKANI ..... 14
27: MAADILI YA UONGOZI ..... 14
28: MAKOSA YA VIONGOZI ..... 14
29: NAMNA YA KUSHUGHULIKIA VIONGOZI WALIOKIUKA MAADILI ..... 15
30: KUFUKUZWA UONGOZI ..... 15
SEHEMU YA SITA: MIKUTANO YA JUVIKIBA ..... 16
31: VIKAO NA MIKUTANO ..... 16
32: MIKUTANO YA TAWI ..... 16
33: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA TAWI ..... 16
34: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI ..... 17
35: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI ..... 17
36: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA TAWI ..... 17
37: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA TAWI ..... 17
38: MIKUTANO YA KATA ..... 18
39: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KATA ..... 18
40: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KATA ..... 18
41: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA KATA ..... 18
42: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA KATA ..... 19
43: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA KATA ..... 19
44: MIKUTANO YA JUVIKIBA WILAYA ..... 19
45: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA WILAYA ..... 20
46: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WILAYA ..... 20

47: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA WILAYA ........................................ 20
48: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA WILAYA ........................................ 21
49: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA WILAYA ........................................ 21
50: MIKUTANO YA JUVIKIBA MKOA ........................................ 21
51: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA MKOA ........................................ 22
52: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA ........................................ 22
53: MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA ........................................ 22
54: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA MKOA ........................................ 22
55: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA MKOA ........................................ 23
56: MIKUTANO YA JUVIKIBA TAIFA ........................................ 23
57: WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA JUVIKIBA TAIFA ........................................ 23
58: MKUTANO MKUU WA MWAKA WA JUVIKIBA TAIFA ........................................ 24
59: KAZI ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA- JUVIKIBA TAIFA ........................................ 24
60: MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA JUVIKIBA TAIFA ........................................ 24
61: MKUTANO MKUU WA DHARURA WA JUVIKIBA TAIFA ........................................ 25
62: KUTOHUDHURIA VIKAO ........................................ 25
SEHEMU YA SABA: UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA JUVIKIBA ........................................ 26
63: UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI ........................................ 26
64: KUSHIKILIA NAFASI ZILIZO WAZI ........................................ 27
65: KUKASIMU MADARAKA KWA UONGOZI ........................................ 27
66: KUONDOLEWA KIONGOZI MADARAKANI ........................................ 27
SEHEMU YA NANE:VYANZO VYA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ........................................ 29
67: VYANZO VYA MAPATO ........................................ 29
68: KUPITISHA MAOMBI YA FEDHA ........................................ 29
69: KUTOPITISHA MAOMBI YA FEDHA ........................................ 30
70: KUFUNGUA AKAUNTI ZA JUMUIYA ........................................ 30
71: UKAGUZI WA FEDHA ........................................ 31

SEHEMU YA TISA: UTATUZI WA MIGOGORO NA MABADILIKO YA KANUNI ... 32

72: UTARATIBU WA KUTATUA MIGOGORO ... 32

73: MABADILIKO YA KANUNI ... 32

74: MUHURI WA JUVIKIBA ... 32

75: MASUALA YA DINI ... 33

76: ITHIBATI YA KANUNI ... 33

## UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Katiba ya Bakwata ya Mwaka 1999 Toleo la 2018, Sura ya Sita kifungu kidogo cha 100 kinatamka wazi kuwa: "Jumuiya za Baraza Kuu zitatengeneza Kanuni zake na kupitishwa na kikao cha Halmashauri Kuu ili kupata idhini kabla ya kutumika.

JUMUIYA YA VIJANA WA KIISLAMU BAKWATA (JUVIKIBA) imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya BAKWATA Sehemu ya Sita Ibara ya 101.

Sisi Waislamu wa Tanzania kwa kuwa tunaamini kama Waislamu wengine wote Ulimwenguni, kwamba hakuna apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake, na kwamba Muhammad (s.a.w) ni Mtume wake wa mwisho hapana tena Mtume baada yake;

Kwa kuwa vilevile, kwamba Qur'an na Sunnah ndiyo vitu viwili vikubwa, ambavyo Mtume Muhammad (S.A.W) ameviacha kwa Umma wake kwa kwamba ili tuongoke ni lazima tuvisome, tuvizingatie na tuvifuate bara bara;

Tunaamini na kwa kuwa tunakubali kwamba ni wajibu wetu kuendeleza na kuimarisha ITIKADI yetu, na kwamba kuna haja kubwa ya kukuza na kuimarisha ushirikiano, umoja na undugu miongoni mwa Waislamu nchini, kwa hivyo basi kwa Mujibu wa Katiba ya BAKWATA na Miongozo yake, tumeamua kuunda JUVIKIBA kwa lengo la kuratibu, kusimamia na kuongoza shughuli za vijana katika mambo mbalimbali ya vijana yahusuyo Uislamu, ikiwa ni pamoja na Nyanja za Ibada, Elimu, Michezo yenye kuendana na mila na desturi za Kiislamu, nk.

Kuunganisha vijana wa kiislamu kwa kufanya Makongamano, Semina za kielimu na Mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uelewa katika kuisimamia dini yao;

Kanuni hizi zimetungwa ili kusaidia na kurahisisha uendeshaji wa JUVIKIBA. Hivyo zitatumika kuongoza shughuli za kila siku za Jumuiya. Endapo itatokea kipengele chochote cha kanuni hizi kimekinzana na katiba ya BAKWATA, basi katiba ndio itakayotawala. Wanajumuiya wote wa JUVIKIBA wanawajibika kuzifahamu, kuziheshimu na kuzitumia kanuni hizi ili kufanikisha uendeshaji mzuri na endelevu wa Jumuiya yetu.

## SEHEMU YA KWANZA
## TAARIFA YA KANUNI

**1. JINA LA KANUNI**

Kanuni hizi zitaitwa KANUNI ZA JUMUIYA YA VIJANA WA KIISLAMU BAKWATA ambapo kwa kifupi zitajulikana kama KANUNI ZA JUVIKIBA.

**2. TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA**

Kanuni hizi zimeanza kutumika baada ya kuwasilishwa na kupitishwa na Halmashauri Kuu ya BAKWATA tarehe 18/09/2025 kama ilivyoelekezwa na Katiba ya BAKWATA, SEHEMU YA SITA, Ibara ya 101 na 102.

**3. MATUMIZI YA KANUNI**

Kanuni hizi zitatumiwa na wanajumuiya wa JUVIKIBA. Kanuni hizi zitaanza kutumika baada ya kuwasilishwa na kupitishwa na Halmashauri Kuu ya Bakwata Taifa na ikitokea jambo lolote ambalo halipo kwenye katiba ya BAKWATA na kanuni za JUVIKIBA, Vikao vya juu vya BAKWATA vitatoa ufafanuzi wa jambo hilo kwa mujibu wa utaratibu.

**4. TAFSIRI YA MANENO**

Katika kanuni hizi baadhi ya maneno yametumika na kutakuwa na maana mahususi yaliyomaanisha kama**:-**

(a) BAKWATA- Maana yake ni Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania.

(b) DAAWAH - Maana yake ni kulingania watu katika dini ya Allah.

(c) HALMASHAURI KUU – Maana yake ni Chombo cha Maamuzi baada ya Mkutano Mkuu

(d) JUVIKIBA- Maana yake ni Jumuiya ya Vijana wa Kiislamu BAKWATA.

(e) KATIBU- Maana yake ni katibu wa JUVIKIBA ambaye ndiye Mtendaji mkuu wa Jumuiya

(f) MAADILI-Maana yake ni mwenendo mwema wa viongozi na

wanajumuiya wa JUVIKIBA

(g) MADRASA -Maana yake ni chuo cha dini ya Kiislamu.

(h) MWEKA HAZINA -Maana yake ni mtunza fedha na nyaraka za fedha za JUVIKIBA

(i) MWENYEKITI -Maana yake ni mwenyekiti wa JUVIKIBA ambaye ni kiongozi mkuu wa JUVIKIBA

(j) SUNNAH-Maana yake ni mafundisho na maelekezo ya Mtume Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake).

(k) VIONGOZI WA JUMUIYA -Maana yake ni Mwenyekiti, Katibu, Mweka Hazina na wajumbe wa kamati ya utendaji.

(l) WANAJUMUIYA -Maana yake ni wanajumuiya wanufaika wa JUVIKIB

## SEHEMU YA PILI

## JINA, MAKAO MAKUU NA LUGHA

**5. JINA LA JUMUIYA**

Jina la Jumuiya ni JUMUIYA YA VIJANA WA KIISLAMU BAKWATA kwa kifupi JUVIKIBA.

**6. MAKAO MAKUU YA JUMUIYA**

Makao makuu ya JUVIKIBA yatakuwa Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es salaam mahali ambapo ndipo yalipo Makao makuu ya BAKWATA Taifa. Na kama kutakuwa na Mabadiliko ni vile Mkutano Mkuu wa JUVIKIBA utakavyoamua.

**7. MAWASILIANO**

Mawasiliano yoyote ya Barua au vinginevyo yatatumia anuani ambayo itaridhiwa na kupendekezwa na Kamati kuu ya JUVIKIBA na kuwa ndiyo anuani na mawasiliano rasmi ya Jumuiya.

**8. LUGHA RASMI**

(i) Lugha rasmi itakayotumika kwa mawasiliano yoyote itakuwa ni Kiswahili. Lugha ya Kiarabu na Kiingereza zitakuwa ni lugha ambazo zitatumika kwenye nyaraka nyingine kwa mujibu wa sheria nyinginezo za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania endapo italazimu kufanya hivyo.

(ii) Kama itatokea kutokukubaliana juu ya tafsiri ya maana ya kifungu chochote au neno lolote katika katiba hii, lugha ya uamuzi itakayotumika kumaliza hali ya kutokukubaliana ni KISWAHILI.

**9. NEMBO YA JUMUIYA**

Nembo ya JUVIKIBA itakuwa ni alama ya Msikiti, Kitabu na Taa.

## SEHEMU YA TATU
## AKIDA, HADHI NA MALENGO YA JUVIKIBA

### 10. AKIDA

JUVIKIBA kama jumuiya ya vijana wa kiislamu iliyo chini ya BAKWATA, wanajumuiya wake ni vijana wa kiislamu wanaofuata madhehebu ya Ahalu Sunnah Waljamaa kwa mufundisho ya IMAM SHAFI

### 11. HADHI

Hadhi ya JUVIKIBA itaangukia kwenye SEHEMU YA SITA Ibara ya 101 na 102 ya Katiba ya BAKWATA pamoja na kanuni zake hivyo itajikita kwenye masuala ya kidini, kijamii, kiafya, kielimu, kiutamaduni na kiuchumi na itashirikiana na mamlaka za nchi yetu na Taasisi nyingine za ndani na nje ya nchi bila ya kupingana na malengo ya kuanzishwa kwake na sheria nyingine za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

### 12. MALENGO YA JUVIKIBA

JUVIKIBA chini ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania itakuwa na madhumuni na majukumu yafuatayo:-

a) Kuwaunganisha Vijana wote wa kiislamu wa Tanzania kwa lengo la kuratibu na kusimamia shughuli zote za Dini zinazowahusu vijana

b) Kujenga na kudumisha AMANI kwa kutambua kwamba Vijana ndio nguvukazi ya Taifa na uwepo wa Amani ndio chachu ya maendeleo ya vijana na Taifa kwa julma.

c) Kujenga Ushirikiano kati ya Jumuiya na Jumuiya nyingine zenye kujali Utu, Hadhi na Thamani ya Kijana wa kiislamu katika ujenzi wa Taifa lililo imara.

d) Kuratibu na kusimamia Sherehe za Kidini kwenye Sikukuu za Eid, Maulid na Mwaka mpya wa Kiislamu.

e) Kufanya Semina na Makongamano ya Vijana yenye lengo la kuwaelimisha mambo mbalimbali yanayohusu Dini na Dunia yao.

f) Kuratibu na kusimamia Madarasa za watoto na vijana ili kukuza ufahamu wa dini.

g) Kubuni na kuanzisha miradi ya kiuchumi kwa vijana wa kiislamu, kwani uchumi ni chanzo cha kupata familia imara na yenye kumtumikia Mwenyezi Mungu kwa amani na utulivu

h) Kuanzisha na kusimamia vituo vya huduma ya afya kwani afya bora ni uti wa mgongo wa utendaji kazi wa mwanadamu

i) Kuhakikisha kuwa vijana wanaandaliwa katika misingi ya Uzalendo na kuipenda nchi yao.

j) Kuwaandaa vijana kuwa viongozi safi na bora wa BAKWATA na tanzu zake zote pamoja na Taifa kwa ujumla.

k) Kuhakikisha kuwa vijana wanapewa mafunzo ya utayari ili kuwa wenye uweledi wa kuielezea, kuitetea na kuilinda BAKWATA na viongozi wake.

## SEHEMU YA NNE

### UANAJUMUIYA, HAKI NA WAJIBU

**13. UANAJUMUIYA**

a) Itakuwa ni wajibu wa Kijana wa Kiisalmu mwanaume au mwanamke kujiunga kwenye JUVIKIBA kwa kuandika barua kwenye kamati ya utendaji ya Jumuiya kwenye Msikiti wake na itapitishwa na kamati ya Msikiti wake.

b) Jina la mwanajumuiya litaingizwa kwenye orodha ya wanajumuiya wa JUVIKIBA katika tawi husika.

**14. NAMNA YA KUJIUNGA**

a) Muombaji uwanajumuiya atatakiwa kuomba kujiunga na Jumuiya kwa hiari yake bila kulazimishwa.

b) Muombaji uwanajumuiya aliyekubaliwa atawajibika kulipa ada ya kiingilio iliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa JUVIKIBA Taifa.

c) Muombaji aliyekubaliwa atapewa kitambulisho cha uwanajumuiya.

d) Mwombaji aliyekataliwa uwanajumuiya ataandikiwa barua na Katibu wa tawi husika kuelezwa sababu za kukataliwa kwake.

**15. SIFA ZA MWANAJUMUIYA**

Mwanajumuiya wa JUVIKIBA ni lazima awe na sifa zifuatazo: -

a. Awe muislamu mwanaume au mwanamke mwenye akili timamu

b. Awe na umri wa miaka 15 mpaka miaka 40
c. Awe anashughulishwa na yanayowasibu wana Jumuiya
d. Awe anafanya Ibada ipasavyo
e. Asiwe na sifa zisizofaa kwenye jamii
f. Awe na moyo wa kujitolea katika mambo ya kheri
g. Asijihusishe na mambo ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Uislamu ni HARAMU

## 16. HAKI ZA MWANAJUMUIYA

a. Atakuwa na haki ya kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa JUVIKIBA
b. Atakuwa na haki ya kushiriki shughuli zote za JUVIKIBA
c. Atakuwa na haki ya kujitetea na kutoa maelezo yake mbele ya vikao vya maamuzi endapo kuna mashitaka yaliyotolewa juu yake
d. Atakuwa na haki ya kuheshimu na kuheshimiwa.

## 17. WAJIBU WA MWANAJUMUIYA

Mwanajumuiya wa JUVIKIBA atakuwa na Wajibu ufuatao: -

a. Kupigania Usawa, Haki na Maendeleo ya Vijana wa Kiislamu hapa nchini
b. Kujielimisha na kujiendeleza kupitia JUVIKIBA kwa faida yake na kwa faida ya umma kwa ujumla
c. Kushirikiana kwa dhati na vijana wenzie katika kutoa Elimu sahihi kwa jamii
d. Kushiriki katika shughuli zote za JUVIKIBA
e. Kuwa tayari kujikosoa na kukosolewa kwa hekima kwa maslahi ya JUVIKIBA

## 18. KUONDOLEWA UANACHAMA

a. Mwanajumuiya wa JUVIKIBA atakuwa na hiari ya kujiondoa kuwa mwanajumuiya bila ya kulazimishwa.

(c) Mwanajumuiya anaweza kuondolewa kwenye orodha ya wanajumuiya iwapo atafanya mambo yafuatayo:-

- **i.** Kutengeneza mifarakano na makundi,
- **ii.** Kuwagawa Waislamu (wanajumuiya)
- **iii.** Kuiba mali za JUVIKIBA/BAKWATA na mambo mengine yanayo katazwa na Qur-an na Sunnah.

## 19. KURUDISHWA UANACHAMA

Mwanajumuiya anaweza kurudishiwa uwachama wake ikiwa atajirekesha kwa makosa aliyoondolewa uanachama, ataomba kurudishiwa uanachama kwa barua, atalipa ada, michango na faini za malimbikizo ya ada**.**

## SEHEMU YA TANO
## MUUNDO WA UONGOZI NA VIONGOZI WA JUVIKIBA

### 20. MUUNDO WA UONGOZI

a. Kamati Kuu
b. Mkutano Mkuu
c. Kamati za JUVIKIBA

### 21. SIFA ZA KIONGOZI

Kiongozi yeyote wa JUVIKIBA sharti awe Muislamu, pamoja na kutimiza masharti ya Uanachama kama ilivyoelezwa kwenye kanuni hizi, Kiongozi wa JUVIKIBA sharti awe na sifa zifuatazo: -

a. Awe Muislamu mwenye akili timamu, na awe anao ufahamu juu ya Uislamu
b. Awe na umri wa miaka 20 na kuendelea
c. Awe mwenye shughuli halali inayomwingizia kipato kama vile mkulima, mfanya Biashara, mfanya kazi au mfugaji nk.
d. Awe muadilifu, muaminifu, mkweli kwa JUVIKIBA na anaikubali na kuifuata Katiba ya BAKWATA
e. Awe anayekubali kujisahihisha, kusahihishwa ikiwa hapana budi akubali kuwajibika kwa maslahi ya Umma

### 22. KAMATI KUU

Kutakuwa na kamati kuu ya JUVIKIBA ambayo itaundwa na wajumbe wafuatao:

a) Mwenyekiti
b) Katibu
c) Naibu Katibu Dini wa JUVIKIBA
d) Naibu Katibu Utawala wa JUVIKIBA
e) Mweka Hazina
f) Wajumbe Sita wenye majukumu maalum

## 23. MAJUKUMU YA KAMATI KUU

a) Kusimamia utendaji kazi za kila siku katika ofisi za JUVIKIBA
b) Kupokea na kutekeleza maamuzi na maelekezo/ magizo ya BAKWATA
c) Kusimamia na kuratibu vikao na Mikutano ya Jumuiya
d) Kusimamia, kuratibu na kuandaa ajenda za Mikutano
e) Kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya JUVIKIBA ya mwaka uliopita na kuiwasilisha kwenye Mkutano mkuu wa JUVIKIBA
f) Kuandaa bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa JUVIKIBA.
g) Kuandaa taarifa ya utendaji kazi za JUVIKIBA na kuziwasilisha kwenye Mkutani Mkuu wa JUVIKIBA.

## 24. MAJUKUMU YA VIONGOZI

Viongozi wa JUVIKIBA watakuwa na majukumu yafuatayo:

### I. Mwenyekiti

a) Atakuwa ndiye kiongozi na msimamizi mkuu wa shughuli zote za Taasisi ya JUVIKIBA.
b) Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa mikutano na vikao vyote vya Jumuiya ngazi ya Taifa.
c) Atasimamia utekelezaji wa maazimio ya Mkutano mkuu na Kamati kamati kuu
d) Atahakikisha viongozi wengine wote wanawajibika ipasavyo.
e) Atapendekeza majina sita ya wajumbe wa kamati kuu kwa sheikh Mkuu na muft kwa ajili ya Uteuzi.

### II. Katibu

a) Atakuwa ndiye Mtedaji Mkuu wa jumuiya hii.

b) Ataandaa mikutano/vikao na agenda za mikutano/vikao kwa kushirikiana na Mwenyekiti.

c) Atakuwa mwandishi wa Mihutasari yote ya mikutano na vikao vyote vya Jumuiya

d) Ataandaa, kutuma na kupokea barua zote za Jumuiya.

e) Atakuwa ndie mdhibiti na mtunza siri na nyaraka mbalimbali za Jumuiya

**III. Naibu Katibu Dini wa JUVIKIBA**

a) Atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Katibu katika maswala ya dini.

b) Atafanya kazi yoyote kwa maelekezo ya Katibu.

**IV. Naibu Katibu Utawala wa JUVIKIBA**

a) Atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Katibu katika maswala ya utawala.

b) Atafanya majukumu ya Katibu pale anapokuwa hayupo.

c) Atafanya kazi yoyote kwa maelekezo ya Katibu.

**V. Mweka Hazina**

a) Atakuwa mtunza fedha za Jumuiya hii.

b) Atawajibika kutoa taarifa za fedha za Jumuiya kwa kila mwezi na pale inapohitajika.

c) Atahusika kulipa malipo yote yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

d) Atawajibika kuandaa ripoti ya fedha ya mapato na mtumizi ya mwaka.

## 25. MIIKO YA UONGOZI

a. Ni mwiko kwa kiongozi wa JUVIKIBA kutumia Madaraka aliyopewa na waislamu kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa maana yoyote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa na madaraka hayo

b. Ni mwiko kutoa maelezo, taarifa, au siri za JUVIKIBA kwa mtu au chombo chochote bila idhini ya mamlaka inayohusika (BAKWATA).

c. Ni mwiko kujuhusisha na RUSHWA, kushiriki katika shughuli HARAMU kwa mujibu wa dini na mwongozo wa BAKWATA.

## 26. MUDA WA KUKAA MADARAKANI

Kiongozi yeyote wa JUVIKIBA aliyechaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa kanuni hizi atashika madaraka yake kwa muda wa miaka mitano (5) ya kipindi cha uongozi na anaweza kuchaguliwa au kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) bila ya ukomo endapo bado anazo sifa za kuwa kiongozi wa JUVIKIBA.

## 27. MAADILI YA UONGOZI

Kuhusu viwango vya maadili, ambavyo viongozi wa JUVIKIBA wakati wakiwa Madarakani watafanya kazi kadri iwezekanavyo kujenga na kufuata misingi ya uaminifu, huruma, umakini na kujituma.

## 28. MAKOSA YA VIONGOZI

Viongozi wa JUVIKIBA wanapaswa kuwa waaminifu, hivyo viongozi wataonekana kuwa wakosaji wa nidhamu ikiwa:

a. Watatumia mali za JUVIKIBA kwa maslahi yao.
b. Watajifunza vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

c. Watapatikana na kosa la wizi wa fedha/Mali za JUVIKIBA
d. Kwenda kinyume na maadili ya Uislamu kama vile ulevi, uzinifu n.k.
e. Kiongozi wa JUVIKIBA ikiwa atapatikana na makosa hayo basi atapewa adhabu zifuatazo:-
   i. Kuondolewa kwenye uongozi.
   ii. Kufikishwa mahakamani ikiwa atathibitika kwa ushahidi dhahiri kuiba fedha/mali za JUVIKIBA
   iii. Kuondolewa katika orodha ya wanajumuiya.

## 29. NAMNA YA KUWASHUGHULIKIA VIONGOZI WALIOKIUKA MAADILI

a. Kukitokea jambo lolote la ukiukwaji wa maadili kwa kiongozi yoyote wa Jumuiya ya vijana Bakwata, viongozi hao/huyo atashughulikiwa kwa mujibu wa Katiba ya BAKWATA, SEHEMU YA TANO Ibara ya 97. 1 (a - b),1-2.
b. Kamati ya maadili itapokea tuhuma za viongozi na kujadili na kufanya uchunguzi wa tuhuma zitakazopokelewa.
c. Kamati katika kufanya uchunguzi itatumia busara, weledi na umakini katika uchunguzi wa jambo la ukiukwaji wa maadili litakalowakilishwa.

d. Uchunguzi wa kamati ya Maadili utawasilishwa ofisi ya Katibu wa JUVIKUBA, kisha ripoti itapelekwa kwenye Mkutano kuu kwa ajili ya Maamuzi.

## 30. KUFUKUZWA UONGOZI

Kiongozi aliyethibitika kuwa na makosa yaliyotajwa katika kanuni **20** (2) (a),(b),(c) na (d) atafukuzwa uongozi kwa azimio maalumu litakalojadiliwa na Mkutano Mkuu na Uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

## SEHEMU YA SITA
## MIKUTANO YA JUVIKIBA

### 31. VIKAO NA MIKUTANO

JUVIKIBA itakuwa na mikutano na vikao katika kila ngazi, Kikao cha mwanzo cha JUVIKIBA kitakuwa ni tawi. Kwa mujibu wa kanuni hizi ifahamike kuwa Tawi ni MSIKITI, MADRASA au popote pale ambapo JUVIKIBA wanatekeleza Majukumu yao. Kila mwaka kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka utakaofanyika mwezi Disemba, mkutano mkuu wa kawaida utakaofanyika kila baada ya miezi mitatu, na mkutano mkuu wa dharura utakaofanyika wakati wowote kunapokuwa na jambo la dharura la kujadiliwa.

### 32. MIKUTANO YA TAWI

Kutakuwa na Mikutano ya Tawi ya JUVIKIBA kama ifuatavyo:

a) Mkutano mkuu wa mwaka wa Tawi
b) Mkutano mkuu wa kawaida wa Tawi
c) Mkutano mkuu wa dharura wa Tawi

### 33. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA TAWI

Mkutano mkuu wa tawi wa JUVIKIBA utakuwa na wajumbe wafuatao:

a) Mwenyekiti wa JUVIKIBA wa Tawi
b) Katibu wa JUVIKIBA wa Tawi
c) Mweka hazina wa JUVIKIBA wa Tawi
d) Wajumbe wote wa kamati ya JUVIKIBA wa Tawi
e) Waumini wote wanaoishi katika Tawi husika
f) Kiongozi yeyote wa JUVIKIBA wa ngazi ya juu anayeishi katika Tawi husika
g) Mkutano mkuu wa JUVIKIBA wa tawi ndiyo kikao cha juu cha Masuala yote yanayohusu shughuli za JUVIKIBA katika Tawi kwa mujibu wa Kanuni hii, isipokuwa yale tu ambayo kanuni

hizi yameweka wazi na Katiba ya BAKWATA imeyabainisha katika utekelezaji wake

## 34. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Tawi ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

## 35. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA TAWI

a) Kuchagua viongozi wote wa tawi kama:
   - i. Mwenyekiti wa JUVIKIBA wa Tawi
   - ii. Katibu wa JUVIKIBA wa Tawi
   - iii. Mweka hazina wa JUVIKIBA wa Tawi
   - iv. Wajumbe wawili (2) wa Mkutano Mkuu wa Kata wanaowakilisha Tawi
   - v. Wajumbe watano (5) wa Kamati ya Tawi

b) Kumsimamisha Uongozi kiongozi yoyote wa JUVIKIBA wa Tawi endapo imedhihirika kuwa tabia na matendo yake hayaendani na Qur'an na Sunnah wala na Maadili ya BAKWATA.

## 36. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA TAWI

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Tawi ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

## 37. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA TAWI

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Tawi utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano

Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

**38. MIKUTANO YA KATA**

Kutakuwa na Mikutano ya Kata kama ifuatavyo:-

a) Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kata
b) Mkutano Mkuu wa Kawaida wa Kata
c) Mkutano Mkuu wa Dharura wa Kata

**39. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA KATA**

Mkutano Mkuu wa Kata ndiyo kikao chenye kauli ya mwisho juu ya masuala yote yanayohusu shughuli za JUVIKIBA katika Kata kwa mujibu wa kanuni hii, isipokuwa yale tu ambayo Katiba ya BAKWATA imeyaweka wazi kuwa yatashughulikiwa na Baraza. Wajumbe wa Mkutano mkuu wa JUWAKITA Kata ni:

a. Mwenyekiti wa Kata wa JUVIKIBA
b. Katibu wa Kata wa JUVIKIBA
c. Mweka hazina wa Kata wa JUVIKIBA
d. Wajumbe wawili (2) waliochaguliwa kutoka kila tawi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi
e. Viongozi wote wa Vikao vya juu vya JUVIKIBA wanaoishi katika Kata hiyo

**40. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KATA**

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kata ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

**41. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA KATA**

Kutakuwa na Mkutano mkuu wa Kata utakakuwa na Mamlaka yafuatayo: -

a. Kujadili shughuli za maendeleo ya JUVIKIBA kwenye Kata kwa mwaka.

b. Kuchagua Viongozi wa JUVIKIBA katika Kata ambao ni:
   i. Mwenyekiti wa JUVIKIBA wa Kata
   ii. Katibu wa JUVIKIBA wa Kata
   iii. Mweka hazina wa Kata
   iv. Wajumbe wawili (2) wa Mkutano Mkuu wa Wilaya

c. Kupitia, kujadili na kutolea maamuzi malalamiko au maazimio toka vikao vya chini

## 42. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA KATA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Kata ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

## 43. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA KATA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Kata utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

## 44. MIKUTANO YA JUVIKIBA WILAYA

Katika ngazi ya Wilaya JUVIKIBA itakuwa na mikutano ifuatayo:-

i. Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wilaya
ii. Mkutano Mkuu wa Kawaida wa Wilaya
iii. Mkutano Mkuu wa Dharura wa Wilaya

## 45. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA WILAYA

Mkutano mkuu wa wilaya ndiyo kikao chenye kauli ya mwisho kwa mujibu wa kanuni hizi juu ya shughuli zote za JUVIKIBA, isipokuwa yale ambayo Katiba ya BAKWATA imeeleza vinginevyo. Mkutano mkuu wa Wilaya utakaokuwa na wajumbe wafuatao: -

a. Mwenyekiti wa Wilaya wa JUVIKIBA
b. Katibu wa Wilaya wa JUVIKIBA
c. Mweka hazina wa Wilaya wa JUVIKIBA
d. Wenyeviti wote wa JUVIKIBA wa Kata
e. Makatibu wote wa JUVIKIBA wa Kata
f. Wajumbe wawili wa Mkutano Mkuu wa Wilaya kutoka kila Kata ya Wilaya
g. Wajumbe wa vikao vya juu wa JUVIKIBA wanaoishi katika wilaya hiyo

## 46. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WILAYA

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wilaya ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

## 47. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WILAYA

Mkutano Mkuu wa JUVIKIBA Wilaya ndiyo kikao chenye kauli ya mwisho katika wilaya husika kwa mujibu wa Kanuni hizi, labda pale ambapo imeeleza wazi kwenye Katiba ya BAKWATA. Mkutano Mkuu wa Wilaya utakuwa na mamlaka yafuatayo:-

a. Kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti wa JUVIKIBA Wilaya
b. Kupokea uteuzi wa Katibu wa JUVIKIBA Wilaya
c. Kuajiri Mweka hazina/Mhasibu wa Wilaya
d. Kuchagua wajumbe wawili (2) watakao wakilisha Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka wilaya
e. Kuchagua wajumbe saba (7) wa Kamati ya JUVIKIBA Wilaya
f. Kujadili na kupanga shughuli za JUVIKIBA kwenye Wilaya

g. Kufanya Tathimini ya Mipango ya shughuli za JUVIKIBA katika wilaya

h. Kupokea na kuidhinisha Makisio ya Mapato na Matumizi ya Wilaya mwaka hadi mwaka

i. Kumsimamisha, Kumfukuza Kiongozi yoyote wa JUVIKIBA Wilaya itakapodhihirika kwamba matendo yake na tabia yake hayalingani na Qur'an na Sunnah

**48. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA WILAYA**

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Wilaya ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

**49. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA WILAYA**

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Wilaya utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

**50. MIKUTANO YA JUVIKIBA MKOA**

Katika ngazi ya Mkoa JUVIKIBA itakuwa Mikutano na vikao vifuatavyo:-

a) Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mkoa
b) Mkutano Mkuu wa Kawaida wa Mkoa
c) Mkutano Mkuu wa Dharura wa Mkoa

## 51. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA MKOA

i. Mwenyekiti wa JUVIKIBA Mkoa
ii. Katibu wa JUVIKIBA Mkoa
iii. Mweka hazina wa JUVIKIBA Mkoa
iv. Wajumbe wawili toka kila wilaya ya mkoa huo
v. Wajumbe wa vikao vya juu wanaoishi katika mkoa huo
vi. Wenyeviti na Makatibu wote wa Wilaya za Mkoa huo

## 52. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mkoa ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka.

## 53. MAMLAKA YA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA MKOA

a. Kufanya uchaguzi za Mwenyekiti wa JUVIKIBA Mkoa
b. Kupokea teuzi za Katibu wa JUVIKIBA Mkoa
c. Kuajiri Mweka hazina/ Mhasibu wa JUVIKIBA Mkoa
d. Kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wa JUVIKIBA, kuandaa mpango kazi wa kila mwaka wa mkoa na kuandaa taarifa za utekelezaji za mpangokazi huo.
e. Kuwachagua wajumbe kumi (10) watakao ingia kwenye kamati kuu ya Mkoa
f. Kuandaa, kupokea na kuidhinisha Makisio ya mapato na matumizi ya mkoa mwaka hata mwaka
g. Kufanya Tathimini ya Mipango ya shughuli za JUVIKIBA kwenye Mkoa
h. Kuwasimamisha Viongozi kwa ngazi ya mkoa endapo itajiridhisha kuwa matendo na mwenendo wake havilingani na Qur'an na Sunnah wala maadili ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA)

## 54. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA MKOA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa Mkoa ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano

Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

**55. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA MKOA**

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa Mkoa utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

**56. MIKUTANO YA JUVIKIBA TAIFA**

Kutakuwa na Mikutano mikuu mitatu (3) kama ifuatavyo:-

a. Mkutano Mkuu wa Mwaka
b. Mkutano Mkuu wa Kawaida
c. Mkutano Mkuu wa Dharura

**57. WAJUMBE WA MKUTANO MKUU WA JUVIKIBA TAIFA**

Mkutano Mkuu wa JUVIKIBA wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao: -

a) Mwenyekiti wa JUVIKIBA Taifa
b) Katibu JUVIKIBA Taifa
c) Manaibu Katibu JUVIKIBA Taifa
d) Wajumbe wa Kamati kuu JUVIKIBA Taifa
e) Wajumbe watatu (3) kutoka kila Mkoa
f) Wajumbe kumi (10) walioteuliwa na Mwenyekiti
g) Wenyeviti na makamu wote wa JUVIKIBA Mkoa na Wilaya
h) Makatibu na manaibu wote wa JUVIKIBA Mkoa na Wilaya
i) Waweka Hazina wote wa JUVIKIBA Mkoa na Wilaya

## 58. MKUTANO MKUU WA MWAKA WA JUVIKIBA TAIFA

Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa JUVIKIBA Taifa ambao utafanyika mwezi Disemba ya kila mwaka. Mkutano Mkuu wa JUVIKIBA Taifa utakuwa ndicho kikao kikuu kupita vyote vya JUVIKIBA.

## 59. KAZI ZA MKUTANO MKUU WA MWAKA-JUVIKIBA WA TAIFA

a) Kupokea teuzi za viongozi wa juu wa Jumuiya ambao ni Mwenyekiti na Katibu.

b) Kuajiri Mweka hazina/Mhasibu wa JUVUKIBA Taifa

c) Kuchagua wajumbe watano (5) wa Kamati Kuu ya JUVIKIBA Taifa

d) Kukiagiza kikao chochote cha JUVIKIBA katika ngazi zote kufanya kazi zozote ambazo Mkutano Mkuu utaona inafaa

e) Kubadili au kuongeza chochote kwenye Kanuni za JUVIKIBA kwa maelekezo ya Halmashauri kuu Taifa na mamlaka za juu nyingine za BAKWATA Taifa.

f) Utapokea na kujadili taarifa ya kazi za JUVIKIBA zilizoandaliwa na Kamati Kuu na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa mujibu wa taratibu za BAKWATA zinazohusu Maendeleo ya Vijana na Mipango ya JUVIKIBA.

## 60. MKUTANO MKUU WA KAWAIDA WA JUVIKIBA TAIFA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Kawaida wa JUVIKIBA Taifa ambao utahudhuriwa na wajumbe waliotajwa kwenye Mkutano Mkuu kujadili maendeleo ya Jumuiya kwa kipindi cha miezi mitatu.

b) Mkutano huu utafanyika kila baada ya miezi mitatu (3) tokea tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mwaka kufanyika.

## 61. MKUTANO MKUU WA DHARURA WA JUVIKIBA TAIFA

a) Kutakuwa na Mkutano wa Dharura wa JUVIKIBA Taifa utakaoitishwa wakati wowote kunapokuwa na jambo la kujadiliwa kwa dharura.

b) Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu kujadili jambo muhimu la dharura tu, ambalo haliwezi kusubiri Mkutano Mkuu wa Mwaka au ule wa Kawaida.

## 62. KUTOHUDHURIA VIKAO

a. Mwanajumuiya asipofika kwenye vikao bila taarifa atakuwa amefanya kosa ambalo atachukuliwa hatua.

b. Mwanajumuiya asipofika kwenye vikao viwili mfululizo bila taarifa atapewa onyo na mara ya tatu asipohudhuria anaweza kuondolewa uanachama na kufutwa kwenye daftari la uwanajumuiya

## SEHEMU YA SABA

## UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA JUVIKIBA

### 63. UTEUZI NA UCHAGUZI WA VIONGOZI

Kutakuwa na viongozi wa kuteuliwa na kuchaguliwa kwa utaratibu ufuatao:

a) Uteuzi wa viongozi utafanyika kila baada ya miaka mitano (5) baada ya viongozi waliokuwa madarakani kumaliza muda wao.

b) Uteuzi wa Mwenyekiti wa JUVIKIBA Taifa utafanywa na na Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania.

c) Mwenyekiti wa JUVIKIBA ngazi za Mikoa na Wilaya watachaguliwa kwa kupigiwa kura na Mkutano Mkuu wa ngazi husika.

d) Uteuzi wa Makatibu na Manaibu Katibu wa JUVIKIBA Taifa, Mikoa na Wilaya utafanywa na Katibu Mkuu wa BAKWATA.

e) Mweka Hazina (Mhasibu) wa JUVIKIBA katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa watakuwa ni waajiriwa.

f) Viongozi wote wa JUVIKIBA katika Kata na Matawi watachaguliwa na Mkutano Mkuu katika ngazi husika.

g) Uchaguzi utasimamiwa na kamati ya uchaguzi itakayoundwa kwa mujibu wa sheria na kwa kazi hiyo tu. Kamati hiyo itakuwa na Mwenyekiti, katibu na wajumbe watatu.

h) Katika chaguzi za Viongozi, mshindi ni yule atakayepata kura nyingi zaidi.

i) Katika chaguzi, kura zitakazopigwa zitakuwa ni kura za siri

j) Kamati ya uchaguzi ndio chombo kitakachosimamia uchaguzi katika hatua zote na kwamba baada ya kumaliza zoezi la kupiga na kuhesabu kura mshindi atatangazwa katika eneo ambalo uchaguzi umefanyika.

k) Kutakuwa na Mawakala wa kila mgombea wakati wa kuhesabu kura.

l) Uchaguzi wa marudio utafanyika ikiwa wagombea watalingana kwa kura, ikiwa kura zitalingana kwa mara ya pili, mwenyekiti wa JUVIKIBA katika ngazi husika atakuwa na kura ya turufu.

m) Mgombea anaweza kukata rufaa katika ngazi za juu kwa kujaza fomu maalum ndani ya masaa 24 baada ya kutangazwa matokeo.

### 64. KUSHIKILIA NAFASI ZILIZO WAZI

Iwapo nafasi katika wadhifa wowote wa JUVIKIBA itabaki wazi kutokana na moja ya sababu zilizoorodheshwa katika Kanuni hii, iwapo aliyekosekana ni kiongozi basi Naibu atashika nafasi lakini iwapo aliyekosekana ni Naibu basi nafasi hiyo itaendelea kubaki wazi mpaka uteuzi au uchaguzi utakapofanyika.

### 65. KUKASIMU MADARAKA KWA UONGOZI

Endapo Mwenyekiti hatakuwepo, atakasimu madaraka yake kwa Makamu Mwenyekiti na kama wote watakuwa hawapo aidha kwa kujiuzulu au kwa dharura yoyote, atateuliwa Mwenyekiti wa muda kukaimu madaraka hayo. Uteuzi au uchaguzi utafanyika ndani ya siku 90 ili kuziba nafasi hiyo.

### 66. KUONDOLEWA KIONGOZI MADARAKANI

Kiongozi yoyote anaweza kuondolewa madarakani kabla ya muda wake wa uongozi kuisha endapo atapoteza sifa za kuwa kiongozi kwa mujibu wa kanuni hii. Baadhi ya sababu za kiongozi kuondolewa madarakani ni kama zifuatazo:

a) Kubadili dini

b) Kurukwa na akili

c) Kufanya matendo maovu kinyume na mafundisho ya Uislamu.

d) Kutohudhuria mikutano na au vikao vitatu mfululizo bila ya ruhusa maalum.

e) Ubadhirifu wa fedha au wizi wa mali za JUVIKIBA

## SEHEMU YA NANE

## VYANZO VYA MAPATO NA KANUNI YA FEDHA

### 67. VYANZO VYA MAPATO

a) Michango ya hiari ya wanajumuiya

b) Mapato kutokana na miradi ya Kiuchumi

c) Ruzuku na Misaada kutoka kwa wahisani na wafadhili

### 68. KUPITISHA MAOMBI YA FEDHA

**a.** Maombi yote ya kuomba fedha yatapitishwa kwa Umakini kwa kuzingatia shida na umuhimu wa fedha inayoombwa.

b. Maombi ya kuomba fedha ya Kutekeleza miradi ya JUVIKIBA, itapitiwa na Katibu na kuthibitishwa na Mwenyekiti.

c. Hati ya Maombi ya fedha (Requisition) kwa ajili ya matumizi ya kawaida (consumable/ service) itajazwa na muombaji ikiambatanishwa na profoma invoice na kuipitisha kwa kiongozi wake wa kamati kwa ajili ya uthibitisho.

d. Hati hiyo itapelekwa kwa Mwenyekiti kwa ajili ya kupata kibali cha matumizi.

e. Muweka Hazina atakagua nyaraka zote kuhakikisha kuwa zipo sawa ndipo atafanya malipo.

f. Muombaji ataitia saini hati ya malipo kabla ya kukabidhiwa pesa.

g. Muombaji ataenda kununua kitu alichokiomba na kukiambatanisha na stakabadhi ya manunuzi kuthibitisha kafanya manunuzi na kuirudisha kwa Mweka Hazina.

h. Muweka Hazina atamsainisha hati ya mapokezi (goods Received Voucher) na kuambatanisha risiti na hati ya malipo.

i. Taratibu kama hizo zitafuatwa kwa manunuzi ya mali (Capital goods) isipokuwa Muweka Hazina atahakikisha kuwa kinachonunuliwa kipo katika bajeti.

j. Mwenyekiti na kamati yake ya fedha watajadili na kuyapitisha maombi hayo ya fedha baada ya kupitishwa na Mkutano Mkuu.
k. Mweka Hazina atawajibika kutunza taarifa zote za fedha na kuzitolea ufafanuzi atakapotakiwa kufanya hivyo na Mkutano Mkuu, wakaguzi wa hesabu au mkutano wowote.
l. Mwenyekiti na kamati yake ya fedha watajadili na kuyapitisha maombi hayo ya fedha baada ya kupitishwa na Mkutano.
m. Mweka Hazina atawajibika kutunza taarifa zote za fedha na kuzitolea ufafanuzi atakapotakiwa kufanya hivyo na Mkutano Mkuu, wakaguzi wa hesabu au mkutano wowote.

## 69. KUTOPITISHA MAOMBI YA FEDHA

a) Tahadhari kubwa itachukuliwa katika kupitisha maombi ya fedha ili kudhibiti mianya ya ubadhirifu wa fedha za JUVIKIBA.
b) Maombi yoyote ya fedha yasiyofuata utaratibu uliowekwa hayatapitishwa au kushughulikiwa.
c) Utaratibu wa kuomba fedha ni sharti ufuatwe ili kujiridhisha na uhalali wa maombi hayo.
d) Mweka Hazina atawajibika kutunza taarifa zote za fedha kuzitolea ufafanuzi atakapotakiwa kufanya hivyo na mkutano mkuu au mkutano wowote au kikao chochote pamoja na ukaguzi.

## 70. KUFUNGUA AKAUNTI ZA JUMUIYA

a) Fedha zote za JUVIKIBA zitatunzwa katika benki itakayokubalika na wanajumuiya.
b) Malipo ya fedha yote yatafanyika kwa kutumia hundi ambazo zitasainiwa kundi A na kundi B ambao watatokana na viongozi wa juu.

c) Muweka Hazina anaweza kutunza nyaraka nyeti za fedha ndani ya Kasha (Safe).

d) Ufunguo wa Kasha utatunzwa na Muweka Hazina.

e) Mweka Hazina atawajibika kuandaa taarifa za fedha kila mwaka na kutoa taarifa kwenye vikao vya kawaida na Mkutano Mkuu.

**71. UKAGUZI WA FEDHA**

**a.** Ukaguzi wa ndani utafanywa na wajumbe watakaoteuliwa na Kamati kuu.

**b.** Mkaguzi wa nje atachaguliwa na Mkutano Mkuu na kufanya kazi kwa uhuru bila ya kuingiliwa**.**

c. Mkaguzi wa nje atawajibika kuandaa taarifa za ukaguzi wa fedha na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu.

d. Mkaguzi wa nje ni sharti awe Mhasibu aliyesajiliwa na Bodi ya Wahasibu ya Taifa.

## SEHEMU YA TISA
## UTATUZI WA MIGOGORO NA MABADILIKO YA KANUNI

### 72. UTARATIBU WA KUTATUA MIGOGORO

Kutakuwa na Kamati ya Maadili itakayoteuliwa na Mkutano mkuu na kuwajibika kwa Kamati Kuu. Kamati ya Maadili itakuwa na wajumbe watatu na itakuwa ndio chombo cha usimamizi wa nidhamu na utatuzi wa migogoro.

(i) Migogoro yote ya kiutendaji au uongozi itashughulikiwa na kamati ya maadili.

(ii) Endapo suluhu haitapatikana mgogoro huo utapelekwa kwenye Kamati kuu na kisha kwenye Mkutano mkuu kwa hatua zaidi.

(iii) Upande ambao hautaridhika na maamuzi hayo utakata rufaa kwenye ngazi ya juu kwa mamlaka iliyowateua.

(iv) Wakati wa kujadili jambo lolote ambalo linamgusa kiongozi yeyote kwenye kamati ya uongozi ikionekana ni busara kiongozi huyo ataombwa kutoka nje ili ajadiliwe.

(v) Ikiwa jambo linalobishaniwa ni la kidini BAKWATA ngazi husika wataombwa kutoa muongozo ambao utakuwa ni wa mwisho.

### 73. MABADILIKO YA KANUNI

Kubadili kanuni za Jumuiya kutafanywa na wanajumuiya wenyewe na watapiga kura ya kukubali kubadilisha vipengele vya kanuni. Mabadiliko ya kanuni yataanza kutumika baada ya kupata idhini ya Mkutano wa Halmashauri kuu ya BAKWATA Taifa.

### 74. MUHURI WA JUVIKIBA

Kutakuwa na mihuri mbalimbali ya **JUVIKIBA** kutokana na idara na mahitaji mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Muhuri wa JUVIKIBA (Huu ni muhuri wa Jumuiya ambapo utasomeka kwa jina la JUMUITA YA VIJANA WA KIISLAMU BAKWATA TAIFA na utakuwa chini ya Katibu wa JUVIKIBA

(ii) Muhuri wa Jumuiya kwa ngazi zinazofuata ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata hadi Msikiti utagongwa kwenye nyaraka za Jumuiya kwa ngazi husika. Muhuri huu utasomeka kwa jina la JUMUIYA YA VIJANA WA KIISLAMU BAKWATA (JUVIKIBA)

## 75. MASUALA YA DINI

Masuala ya dini katika JUVIKIBA yatasimamiwa na viongozi wa dini kama Ustadh, Imamu na Sheikh.

## 76. ITHIBATI YA KANUNI

Kanuni hizi zimethibitishwa na Halmashauri Kuu BAKWATA Taifa kwa mujibu wa Ibara ya 101 na 102 za Katiba ya BAKWATA ya Mwaka 1999, toleo la mwaka 2018.